ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 45*** ***6th November, 2020***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette Of The United Republic Of Tanzania No 45 Vol.101 Dated 6th November, 2020*
Printed By The Government Printer, Dodoma By Order Of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 975 La Tarehe 6/11/2020

SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA,
[SURA YA 398]

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 31(1) na (2)(f))*

SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA (AHADI YA UADILIFU) KANUNI, 2020

## MPANGILIO WA VIFUNGU

### SEHEMU YA KWANZA
### VIFUNGU VYA AWALI

*Kifungu* *Jina*

1. Jina.
2. Matumizi ya Kanuni.
3. Ufafanuzi wa maneno.

### SEHEMU YA PILI
### MALENGO NA MISINGI YA AHADI YA UADILIFU

4. Malengo ya Ahadi ya Uadilifu.
5. Misingi ya Ahadi ya Uadilifu.

### SEHEMU YA TATU

## WAJIBU WA VIONGOZI WA UMMA

6. Kusaini Ahadi ya Uadilifu.
7. Masharti ya kuzingatiwa na Viongozi wa Umma.
8. Kiongozi wa Umma kuzingatia masharti ya ahadi ya uadilifu.

## SEHEMU YA NNE
## UFUATILIAJI NA USIMAMIZI

9. Wajibu wa Sekretarieti.
10. Uchunguzi.
11. Mamlaka ya Kamishna.
12. Ukiukaji wa Kanuni.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI MENGINEYO

13. Ahadi ya uadilifu iliyosainiwa kabla.

SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA,
[SURA YA 398]

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 31(1) na (2)(f))*

SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA (AHADI YA UADILIFU) KANUNI, 2020

## SEHEMU YA KWANZA
## VIFUNGU VYA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Ahadi ya Uadilifu), 2020.

Matumizi ya Kanuni

2. Kanuni hizi zitatumika kwa Viongozi wote wa Umma.

Ufafanuzi wa maneno

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa tu pale ambapo itahitajika vinginevyo-

Sura ya.398

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

"Kamishna" ina maana kama ilivyofafanuliwa katika Sheria;

Sura ya 1

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977;

"ahadi ya uadilifu" maana yake ni tamko rasmi la kimaandishi linalotolewa na viongozi wa umma kuonesha dhamira ya kuzingatia misingi ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa;

"Kiongozi wa Umma" ina maana kama ilivyofafanuliwa na Sheria;

"Sekretarieti" ina maana kama ilivyofafanuliwa na kifungu cha 18(1) cha Sheria;

"uzalendo" maana yake ni hali ya mtu kuipenda sana nchi

yake kiasi cha kuwa tayari kufa kwa ajili ya kuitetea;

"Maadili" ina maana kama ilivyofafanuliwa katika Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## MALENGO NA MISINGI YA AHADI YA UADILIFU

Malengo ya ahadi ya uadilifu

4. Malengo ya ahadi ya uadilifu yatakuwa ni:

(a) kuhamasisha viongozi kuishi na kuwa na mwenendo wa kimaadili;
(b) kutoa nafasi kwa Viongozi wa Umma ya kujitathmini wenyewe;
(c) kuhamasisha hali ya Viongozi wa Umma kujidhibiti wenyewe;
(d) kuongeza imani ya wananchi kuhusu uadilifu wa viongozi wa umma na utaratibu mzima wa kutoa maamuzi ya Serikali; na
(e) kujenga utamaduni wa uadilifu ambao unawahimiza Viongozi wa Umma kuishi na kuamini katika misingi ya Utawala Bora.

Misingi ya ahadi ya uadilifu

5. Ahadi ya uadilifu itajenga na kutekeleza misingi ifuatayo ya maadili:

(a) uwazi katika utekelezaji wa shughuli za umma na kufanya maamuzi;
(b) uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya umma;
(c) uadilifu katika utendaji wa kazi za umma na utaratibu wa kutoa maamuzi ya Serikali na Sekta ya Umma;
(d) weledi;
(e) uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu;
(f) uzalendo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
(g) uaminifu katika shughuli za umma ili kulinda fedha na mali nyinginezo za umma; na
(h) kuepuka mgongano wa maslahi.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU WA VIONGOZI WA UMMA

Kusaini ahadi ya uadilifu

6. Kila Kiongozi wa Umma, isipokuwa pale ambapo Katiba au sheria nyingine itaeleza vinginevyo, atasaini mbele ya Kamishna nakala mbili za Hati ya Ahadi ya Uadilifu katika fomu kama inavyoonekana katika Jedwali la Kanuni hizi.

(2) Kiongozi wa Umma atasaini ahadi ya uadilifu mara moja wakati akitumikia wadhifa wake.

(3) Kiongozi wa Umma atasaini ahadi mpya ya uadilifu mara tu baada ya kuteuliwa au kupandishwa cheo.

(4) Ahadi ya uadilifu iliyojazwa na kusainiwa itawasilishwa kwa Kamishna ambaye atabaki na nakala moja na nakala nyingine itarudishwa kwa Kiongozi husika.

(5) Kwa madhumuni ya kanuni hii neno "Kamishna" linajumuisha wawakilishi wake walioteuliwa kutekeleza majukumu kwa niaba ya Kamishna.

Masharti ya kuzingatiwa na Viongozi wa Umma

7. Kila Kiongozi wa Umma mwenye kushika wadhifu ulioainishwa kwenye Sheria atapaswa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) kuwa mzalendo na mtii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) kuwa muadilifu na mfano kwa watumishi wa umma, watumishi wa Bunge, watumishi wa Mahakama na watu wengine katika kukuza na kusimamia maadili;

(c) kutotumia cheo chake kwa maslahi binafsi au ya familia yake, ndugu zake, marafiki zake au mtu mwingine tofauti na maslahi ya umma;

(d) kulinda na kutumia rasilimali za umma kwa maslahi ya umma;

(e) kutumia mamlaka na kutoa maamuzi kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni, taratibu, miongozo, mila na desturi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(f) kutotenda vitendo vya rushwa;

(g) kutoomba, kutoa au kupokea zawadi au manufaa yasiyoruhusiwa na sheria;
(h) kujiepusha kutoa shinikizo linalokiuka sheria, kanuni, taratibu na miongozo katika kutekeleza majukumu ya umma;
(i) kutotoa kwa mtu asiyehusika taarifa zozote za siri zinazopatikana wakati wa kutekeleza majukumu yake rasmi kinyume na sheria;
(j) kutekeleza majukumu rasmi kwa kuepuka mgongano wa maslahi na wakati wote kufanya uamuzi kwa kuzingatia Katiba na sheria;
(k) kutumikia watu wote kwa usawa bila kuwabagua kwa misingi ya dini, siasa, kabila, udugu, ukanda, jinsia au hali ya mtu; na
(l) kuheshimu nafasi ya uongozi wa umma akiwa mahali pa kazi, nje ya mahali pa kazi au baada ya kustaafu au kuacha kazi.

Kiongozi wa Umma kuzingatia masharti ya ahadi ya uadilifu

8.-(1) Kiongozi wa umma katika kipindi chake chote cha utumishi atapaswa kuzingatia masharti ya ahadi ya uadilifu.

(2) Kiongozi wa umma hapaswi kukiuka matakwa ya ahadi ya uadilifu

## SEHEMU YA NNE
## UFUATILIAJI NA USIMAMIZI

Wajibu wa Sekretarieti

9. Sekretarieti ina wajibu wa kuhakikisha uzingatiaji wa Kanuni hizi kwa:
(a) kuhakikisha kuwa viongozi wa umma wanatia sahihi Hati ya Ahadi ya Uadilifu;
(b) kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa ahadi ya uadilifu;
(c) kufanya uchunguzi kubaini iwapo Kiongozi yeyote wa Umma amekiuka vifungu vya Kanuni hizi; na
(d) kufanya mambo yote muhimu katika kusimamia kanuni hizi.

Uchunguzi

10. Kwa kuzingatia kifungu cha 18 cha Sheria,

Kamishna anaweza, kwa madhumuni ya utekelezaji wa kanuni hizi kuanzisha uchunguzi dhidi ya Kiongozi wa Umma kwa ukiukaji wa ahadi ya uadilifu.

Mamlaka ya Kamishna

11. Kamishna ana mamlaka ya:

(a) kumwita na kumtaka mtu yeyote kuwasilisha au kutoa taarifa yoyote ambayo anaona ni muhimu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria; na
(b) kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria katika kusimamia utekelezaji wa matakwa ya Kanuni hizi.

Ukiukaji wa Kanuni

12. Kiongozi wa umma ambaye atakiuka vifungu vya kanuni hizi atakuwa amekiuka maadili ya Viongozi wa Umma na atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na sheria nyingine za nchi.

## SEHEMU YA TANO
## MAMBO MENGINEYO

Ahadi ya audilifu iliyosainiwa kabla

13. Viongozi wote wa umma ambao hapo awali walitia saini Ahadi ya Uadilifu chini ya Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma, namba 2 wa mwaka 2015 watahesabika kuwa wametia saini Ahadi ya Uadilifu chini ya Kanuni hizi.

---

JEDWALI

---

**PL. 3**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

---

SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA
AHADI YA UADILIFU KWA VIONGOZI WA UMMA

Kwa kuzingatia misingi ya maadili iliyoainishwa katika Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995, ambayo yanamtaka kila kiongozi wa umma kuzingatia viwango vya juu vya maadili ili kukuza utu, uwazi, uadilifu, uwajibikaji na kuimarisha imani ya wananchi kuhusu utendaji wa viongozi wa umma.

Mimi, .............................................................. ninauahidi umma kwamba:

1. Nitakuwa mzalendo na mtii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
2. Nitakuwa muadilifu na mfano kwa watumishi wa umma, watumishi wa Bunge, watumishi wa Mahakama na watu wengine katika kukuza na kusimamia maadili;
3. Sitatumia cheo changu kwa maslahi binafsi au ya familia yangu, ndugu zangu au marafiki zangu au mtu mwingine;
4. Nitalinda na kutumia rasilimali za umma kwa maslahi ya umma;
5. Nitatekeleza majukumu yangu na kufanya maamuzi kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni, taratibu, miongozo, mila na desturi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
6. Sitatenda kitendo chochote cha rushwa;

7. sitaomba, kutoa au kupokea zawadi au fadhila isipokuwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na sheria;
8. Sitatoa shinikizo linalokiuka sheria, kanuni, taratibu na miongozo katika utendaji kazi za umma;
9. Sitatoa siri ambazo nitazipata au kuzijua katika utumishi wangu isipokuwa kama sheria itaelekeza vinginevyo;
10. Nitatekeleza majukumu yangu kwa kuepusha mgongano wa maslahi wa aina yoyote na mara zote nitatoa uamuzi kwa kuzingatia Katiba na sheria;
11. Nitatoa huduma bora kwa usawa kwa watu wote bila kujali misingi ya dini, siasa, kabila, udugu, utaifa, ukanda, jinsia au hali ya mtu; na
12. Nitazingatia na kulinda heshima ya nafasi yangu ya uongozi wa umma ninapokuwa kazini, nje ya mahali pa kazi na hata nitakapostaafu au kuacha kazi.

**TAMKO:** Ninakiri kwamba nimeisoma Hati hii ya Ahadi ya Uadilifu kabla ya kuweka saini. Ninakubali na kutambua kwamba masharti yaliyomo katika Hati hii ni ya kimaadili na kisheria na ninawajibika kuyatekeleza. Ninaelewa kwamba kuvunja masharti hayo ni ukiukwaji wa maadili yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na sheria za nchi na hatua za kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi yangu iwapo nitakiuka masharti hayo.

| ............................................ | ........................... | .................. | ................. |
|---|---|---|---|
| Jina | Wadhifa | Saini | Tarehe |

| ............................................................ | ........................... | ...................... |
|---|---|---|
| Kamishna Wa Maadili | Saini | Tarehe |

Dodoma,
23 Oktoba, 2020

GEORGE H. MKUCHIKA
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,*
*Menejimenti*
*ya Utumishi wa Umma na*
*Utawala Bora*